

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990
Telegramu: Railways
Nukushi: 2133428



Ofisi ya Uhusiano
S.L.P 70364
Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA YAH: KANUSHO LA KUZUIWA KWA BEHEWA ZA SGR UJERUMANI

Dar es Salaam, Tarehe 22 Novemba 2022.

Shirika la Reli Tanzania – TRC linakanusha taarifa iliyotolewa katika Gazeti la Jamhuri tarehe 22 Novemba, 2022 yenye kichwa cha habari "**MABEHEWA YA SGR YAZUIWA UJERUMANI**", taarifa hiyo haina ukweli na ina lengo la kupotosha umma kuhusu jitihada zinazofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza na kuboresha Sekta ya miundombinu ya reli nchini.

Mkataba wa matengenezo ya behewa thelathini (30) na vichwa viwili (2) vya treni kati ya Shirika la Reli Tanzania na kampuni ya Euro Wagon ulivunjwa mnamo tarehe 25 Februari 2022 baada ya kampuni kushindwa kukidhi matakwa ya mkataba, hatua iliyopelekea TRC kutafuta mkandarasi mwingine ambaye ni kampuni ya LUECKEMEIER TRANSPORT AND LOGISTICS GMBH ya nchini Ujerumani.

Kazi ya matengenezo ya behewa inaendelea chini ya kampuni ya LUECKEMEIER TRANSPORT AND LOGISTICS GMBH na inaendelea vema. TRC haijapokea taarifa yoyote kuhusu kuzuiwa au kuuzwa kwa behewa kutoka kwa mkandarasi ambaye ni kampuni iliyopewa dhamana ya kuendelea na matengenezo ya behewa.

Shirika la Reli Tanzania linatoa huduma ya usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli, TRC imepewa dhamana ya kujenga, kuendeleza na kusimamia miundombinu ya reli. Kwa sasa TRC inasimamia mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR awamu ya kwanza Dar es Salaam – Mwanza na ujenzi unaendelea vema. TRC inatarajia kupokea behewa za SGR zilizotengenezwa na kampuni Sung Shin Rolling Stock Technology Limited (SSRST) kutoka Korea ya Kusini rasmi tarehe 25 Novemba, 2022 siku ya Ijumaa, hivi sasa behewa hizo zimeshafika Bandari ya Dar es Salaam tayari kwaajili ya kushushwa.

Jamila Mbarouk
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano